



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UCHUKUZI**

CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI



TAARIFA KWA UMMA



UTEUZI WA DKT. PROSPER L. MGAYA KUWA MKUU WA CHUO CHA TAIFA CHA USAFIRISHAJI (NIT)

Tarehe 6 Machi 2024, Dar es Salaam,

Uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) unapenda kuijulisha jumuiya ya NIT na umma kwa ujumla kuwa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, amemteua Mha. Dkt. Prosper Lutangilo Mgaya, kuwa Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, kuanzia tarehe 4 Machi, 2024.

Dkt. Mgaya anachukua nafasi ya Mha. Prof. Zacharia Mganilwa, ambaye amemaliza muda wake tarehe 3 Novemba, 2023 na tangu wakati huo nafasi ya Mkuu wa Chuo ilikuwa ikikaimiwa na Dkt. Zainabu Mshana, ambaye ni Naibu Mkuu wa Chuo - Mipango, Fedha na Utawala.

Kabla ya uteuzi huu Dkt. Mgaya alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Dkt. Mgaya ni Mhandisi mbobevu katika masuala ya Rasilimali Maji (Water Resources Engineering). Vilevile ni Mwenyekiti wa Bodi ya Sayansi na Teknolojia Shirikishi (Science and Allied Technologies) ya Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET).

Uongozi wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji na Wanajumuiya ya NIT wanampongeza Dkt. Mgaya kwa uteuzi huo na kumtakia utendaji kazi bora katika nafasi yake. Vilevile, tunamshukuru Dkt. Zainabu Mshana kwa mchango wake katika kuendeleza shughuli za Chuo kwa bidii na uadilifu katika kipindi chake na tunamtakia kazi njema katika majukumu yake ya Naibu Mkuu wa Chuo – Mipango, Fedha na Utawala.

Imetolewa na

**Tulizo Chusi
Afisa Uhusiano Mkuu**